

## Kondoo na mbuzi waliolishwa vyema

- Hutoa maziwa zaidi
- Hutoa nyama zaidi
- Huzaa wanambuzi na wanakondoo wengi maishani mwao.



Wanyama waliolinzwa vyema



### Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, Nairobi.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

#### Watayarishaji:

Mbuku S.M., Kilitit J.K. na Muhuyi W.B

#### Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

#### Mkuu wa kituo,

KARI- Lanet

S.L.P. 3840, 21000 Nakuru

Simu: 254 51 851217

Baruapepe: karinet@africaonline.com

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 56 /2008

**Shilingi 20 za Kenya**

**Jinsi ya kuwapa mbuzi na kondoo lishe nyongeza kwa kutumia miti asili ya jamii ya kunde katika sehemu kame**



## Utangulizi

Kondoo na mbuzi katika sehemu kame za Kenya hutegemea malisho ya mimmea ya kiasili ambayo huwa na kiasi duni cha protini na nguvu. Hii husababisha uwezo duni wa uzazi, kutokua haraka na utoaji maziwa duni. Ni muhimu basi kuimarisha maakuli yao kwa kuyaongezea protini ambazo hupatikana kutokana na mbegu za kiasili kama vile *Acacia* and *Balanites*.

Mbegu hizi mbili:

- Hupendeza kondoo na mbuzi.
- Huwa na kiwango cha juu cha protini na nguvu na miili yao huzichukua kwa urahisi.

Pandeza *acacia* zinazoweza kuliwa ni kama vile ngozi ya miti, majani na matunda. Zile za *balanites*, ni kama vile pembe za matawi, majani na matunda.

### **Manufaa ya pande za acacia, ya kuhifadhiwa balanites na nyasi zinazoliwa**

Chakula	Maakuli kavu	Protini	Calcium	fosfolasi
Acacia	65	11	2.8	0.006
Balanites	66	15	1.7	0.013
Nyasi	84	7	0.0	0.0

## Manufaa ya kulisha mikunde kwa kondoo na mbuzi

- Mimea ya *acacia* na ya *balanites* hustahimili ukame na hupatikana wakati wowote mwakani.
- Mbegu zilizokaushwa zinaweza kuhifadhiwa wakati wa kianganzi.
- Huwa na protini, vyakula vya nguvu, maadini na vitamini muhimu katika kuimarisha uzazi na kukua.




**Kondoo wenye afya**

## Jinsi ya kutayarisha maakuli ya kuimarisha afya

- Okota ngozi, pembe za matawi, mimea chipukizi, majani na matunda na uyakaushie juani.
- Katakata vipande vidogo na uvisiage ukitumia nyundo au kipigilio.
- Chunga ili kuondoa vipande visivyoweza kuvunjwa na miili ya wanyama.
- Hifadhi maakuli haya ya pembeni kwenye gunia zinazoingiza hewa.

## Kuwalisha kondoo na mbuzi

- Lisha kondoo na mbuzi kwenye malisho ya asili nyakati za mchana.



**Mbuzi wakili shwa kwenye malisho ya kiasili mchana.**

- Rudisha wanyama kutoka malishoni na uwaingize kwenye boma zao za mapumziko hori.
- Wape wanyama waliokomaa gramu 140 za maakuli ya *acacia* na *balanites* na wale wachanga wapewe gramu 70 kila siku ukitumia besheni au bakuli.



**Wanyama wakila acacia na balanites**